TANGAZO LA SERIKALI NA. 240 la tarehe 24/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA YA 355)

**AMRI**

*(Imetengenezwa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA MJI MPYA – NANGOTI YA MWAKA 2023.

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Mji mpya – Nangoti ya Mwaka 2023.

Kutangaza Eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (Mpango wa Urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Kuandaa na kuhifadhi Mipangokina

3. Mipangokina ya eneo lililoainishwa kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M1 yenye majira - nukta 567021MS, 8809386KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa $06^0$ 17'45'' kwa umbali wa kilomita 1.6 hadi kwenye barabara ya Namikupa kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M2 yenye majira - nukta 567199MS, 8807830KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki kwa kufuata barabara ya Namikupa kwa umbali wa kilomita 2.0 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M3 yenye majira - nukta 569393MS, 8807439KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa $29^0$ 59'38'' kwa umbali wa kilomita 2.0 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M4 yenye majira - nukta 568409MS, 8809145KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa $77^0$ 18'27'' kwa umbali wa kilomita 0.7 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M5 yenye majira - nukta 567698MS, 8808985KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa $10^0$ 31'31'' kwa umbali wa kilomita 0.4 hadi kwenye barabara ya Newala - Mtwara kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M6 yenye majira - nukta 567617MS, 8809418KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa kufuata barabara ya Newala - Mtwara hadi ulipoanzia."

Dodoma,
6 Februari, 2023

BANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*